TANGAZO LA SERIKALI Na. …………………….. la tarehe ………..……………..

SHERIA YA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

(Na. 2 ya mwaka 2024)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 26)*

KANUNI ZA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI


*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTAMBULISHO WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

3. Nembo ya Tume.
4. Lakiri ya Tume.

SEHEMU YA TATU
MALI ZA TUME

5. Mali za Tume.
6. Utaratibu wa kupokea, kuhamisha au kuazimisha mali za Tume.

SEHEMU YA NNE
KAMATI YA USAILI

7. Nafasi wazi ya Mjumbe au Wajumbe wa Tume.
8. Majukumu ya Kamati ya Usaili.
9. Sekretarieti ya Kamati ya Usaili.
10. Posho na stahili za wajumbe wa Kamati ya Usaili.

SEHEMU YA TANO
KAMATI YA UCHUNGUZI

11. Sekretarieti ya Kamati ya Uchunguzi.
12. Posho na stahili za wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi.

SEHEMU YA SITA
UTARATIBU WA KUKABIDHI MADARAKA

13. Makabidhiano.

SEHEMU YA SABA
VIKAO VYA TUME

14. Utaratibu wa Vikao vya Tume.

SEHEMU YA NANE
UGAWAJI WA MAJIMBO

15. Jukumu la kugawa majimbo.
16. Vigezo vya kugawa jimbo la uchaguzi.
17. Utaratibu wa kugawa jimbo au kubadilisha jina.

SEHEMU YA TISA
MAADILI YA UTENDAJI YA TUME

18. Maadili ya utendaji kwa Wajumbe wa Tume.
19. Maadili ya utendaji kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi.

SEHEMU YA KUMI
WATUMISHI WA TUME

20. Watumishi wa Tume.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
WAJIBU WA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KWA WANANCHI

21. Elimu ya mpiga kura.
22. Idhini ya maudhui yanayotumika kutoa elimu ya mpiga kura.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
UHUSIANO KATI YA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI NA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

23. Uhusiano wa Tume na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

SEHEMU YA KUMI NA TATU
MASHARTI MENGINEYO

24. Masharti ya fedha.

MAJEDWALI

TANGAZO LA SERIKALI Na…………………….. la tarehe ………………………..

SHERIA YA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

(NA. 2 YA MWAKA 2024)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 26)*

**KANUNI ZA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI ZA MWAKA 2024**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA UTANGULIZI**

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024.

Tafsiri

**2**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"elimu ya mpiga kura" maana yake ni kutoa elimu kuhusu mchakato na taratibu za uchaguzi;

"Kamati ya Uchunguzi" maana yake ni Kamati iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 8(4) cha Sheria;

"Kamati ya Usaili" maana yake ni Kamati iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Sheria;

"Kanuni za Maadili" maana yake ni Kanuni za Maadili kwa Wajumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi zilizoandaliwa chini ya kifungu cha 11 na 18 cha Sheria na kanuni ya 18 na 19;

Sura ya 2

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

"lakiri ya Tume" maana yake ni muhuri wa moto wa Tume unaogongwa kwenye nyaraka kama itakavyoelekezwa na Tume;

"Mjumbe" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume kwa mujibu wa Ibara ya 74 ya Katiba;

"Mkurugenzi wa Uchaguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 17 cha Sheria na itajumuisha mtu ambaye kwa kipindi hicho atakuwa anatekeleza majukumu yoyote ya ofisi hiyo;

"Mwenyekiti" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuongoza Tume na inajumuisha Makamu Mwenyekiti;

"nembo ya Tume" maana yake ni alama au mchoro unaoitambulisha Tume kama ilivyobainishwa kwenye kanuni ya 3;

Na. 2 ya mwaka 2024

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;

"Tume" maana yake ni Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;

"uchaguzi" maana yake ni uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na inajumuisha

uchaguzi mdogo wa Mbunge au Diwani.

## SEHEMU YA PILI
## UTAMBULISHO WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

Nembo ya Tume

**3**. Kutakuwa na nembo ya Tume ya namna na muonekano kama ilivyobainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Lakiri ya Tume

**4.-** (1) Kutakuwa na lakiri ya Tume, itakayotumika katika nyaraka za Tume kama itakavyoelekezwa na Tume.

(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi atatunza na kuhifadhi lakiri ya Tume.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), nyaraka itachukuliwa kuwa halali ikiwa imegongwa lakiri ya Tume na kusainiwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Uchaguzi au Afisa mwingine aliyeidhinishwa kwa niaba ya Mkurugenzi wa Uchaguzi.

(4) Nyaraka yenye lakiri ya Tume au iliyotolewa kwa niaba ya Tume, itatumika kama ushahidi na itachukuliwa kuwa imeandaliwa au kutolewa na Tume, kama itakavyokuwa bila uthibitisho zaidi.

## SEHEMU YA TATU
## MALI ZA TUME

Mali za Tume

**5.-** (1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, Tume kwa jina lake inaweza kujipatia na kumiliki mali zinazohamishika na zisizohamishika.

(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi atasimamia na kutunza mali za Tume.

Utaratibu wa kupokea, kuhamisha au kuazimisha mali za Tume

**6.** Endapo Tume itapokea, itahamisha au itaazimisha mali yoyote ya Tume, masharti ya sheria husika yatazingatiwa.

## SEHEMU YA NNE
## KAMATI YA USAILI

Nafasi wazi ya Mjumbe au Wajumbe wa Tume

**7.-**(1) Endapo kutakuwa na nafasi wazi ya Mjumbe, Mkurugenzi wa Uchaguzi atamtaarifu Rais kuhusu uwepo wa nafasi hiyo.

(2) Baada ya kupokea taarifa ya uwepo wa nafasi wazi ya Mjumbe, Rais ataitisha Kamati ya Usaili.

Majukumu ya Kamati ya Usaili

**8**.-(1) Kamati ya Usaili iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kupendekeza kwa Rais majina matano kwa kila nafasi kwa ajili ya uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume; na

(b) kusaili watu wanaoomba kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume.

(2) Kwa kuzingatia kifungu cha 9(5) cha Sheria, Kamati ya Usaili, ndani ya siku kumi na nne baada ya kuitishwa itatoa tangazo kwa umma kupitia magazeti angalau mawili yenye wigo mpana wa usambazwaji nchini na vyombo vingine vya habari kuwaalika wananchi wenye nia ya kuomba kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume,

kuwasilisha maombi yao kwenye Kamati ya Usaili.

(3) Kamati ya Usaili baada ya kupokea maombi -

(a) itachambua maombi ya watu walioomba kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume;
(b) itaandaa orodha ya majina ya watu wenye sifa kwa kuzingatia vigezo na sifa zilizoainishwa kwa mujibu wa Sheria;
(c) itatoa tangazo la usaili kwa umma kupitia magazeti angalau mawili yenye wigo mpana wa usambazwaji na vyombo vingine vya habari likionesha orodha ya majina ya waombaji, muda, mahali na tarehe ya usaili;
(d) itasaili waombaji; na
(e) baada ya kukamilisha usaili, Kamati itapendekeza kwa Rais majina ya waombaji waliofaulu usaili kwa kuwasilisha majina manne zaidi ya idadi ya nafasi zinazohitajika kujazwa.

(4) Rais atateua Mjumbe au Wajumbe wa Tume kutoka miongoni mwa majina yatakayowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3)(e).

(5) Mkurugenzi wa Uchaguzi ataandaa mafunzo maalum kwa Mjumbe au Wajumbe wapya walioteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (4), kuhusu majukumu na wajibu wao katika Tume.

Sekretarieti ya Kamati ya Usaili

**9.** Katibu wa Kamati ya Usaili atateua watumishi wa umma wasiopungua watano kuwa Wajumbe wa Sekretarieti kwa kuzingatia utaratibu kama ulivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Posho na stahili za wajumbe wa Kamati ya Usaili

**10**. Wajumbe wa Kamati ya Usaili watalipwa posho na stahili nyingine kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo itakayotolewa na Tume. -

## SEHEMU YA TANO
## SEKRETARIETI NA POSHO ZA KAMATI YA UCHUNGUZI

Sekretarieti ya kamati ya Uchunguzi

**11**.-(1) Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi atateua watumishi wa umma waandamizi wasiopungua watano kuwa wajumbe wa Sekretarieti ya Kamati ya Uchunguzi.

(2) Uteuzi wa wajumbe wa Sekretarieti chini ya kanuni ndogo ya (1) utategemea aina ya uchunguzi unaotarajiwa kufanyika.

Posho na stahili za wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi

**12.** Wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi watalipwa posho na stahili nyingine kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo itakayotolewa na Tume.

## SEHEMU YA SITA
## UTARATIBU WA KUKABIDHI MADARAKA

Makabidhiano

**13**.- (1) Endapo mtu atateuliwa kujaza nafasi ya Mwenyekiti aliyemaliza muda wa uongozi, Mkurugenzi wa Uchaguzi ataandaa utaratibu wa makabidhiano ya ofisi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuapishwa.

(2) Makabidhiano yaliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) yatajumuisha nyaraka zenye taarifa muhimu zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya Tume.

## SEHEMU YA SABA
## VIKAO VYA TUME

Utaratibu wa vikao vya Tume

**14.**- (1) Utaratibu wa vikao vya Tume utafanyika kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 12cha Sheria.

(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi ataandaa, ataratibu na kutunza nyaraka za vikao vya Tume.

(3) Tume inaweza kutumia teknolojia wakati wa kuendesha vikao vyake pale itakapoonekana upo umuhimu wa kufanya hivyo.

## SEHEMU YA NANE
## UGAWAJI WA MAJIMBO

Jukumu la kugawa majimbo

**15.**-(1) Kwa kuzingatia Ibara ya 75(1), (2) na (4) ya Katiba, Tume inaweza mara kwa mara na angalau kila baada ya miaka kumi kugawa eneo lolote la Jamhuri ya Muungano kuwa jimbo la uchaguzi.

(2) Eneo lililogawanywa chini ya kanuni ndogo ya (1), litatangazwa kuwa jimbo la uchaguzi baada ya kupata kibali cha Rais.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Tume inaweza kubadili jina la jimbo la uchaguzi kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Kanuni hizi.

Vigezo vya kugawa jimbo la uchaguzi

**16.** Kwa kuzingatia masharti Ibara ya 75 ya Katiba na kifungu cha 10(1)(d) cha Sheria, katika kugawa eneo la jimbo la uchaguzi, Tume itazingatia vigezo vilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

Utaratibu wa kugawa jimbo au kubadilisha jina

**17.**-(1) Katika kugawa jimbo au kubadilisha jina la jimbo, Tume itatoa tangazo kwa umma kuhusu kugawanywa au kubadilishwa kwa jina la jimbo la uchaguzi.

(2) Pale ambapo wananchi wanahitaji jimbo kugawanywa au kubadilishwa jina, watawasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri mapendekezo ya kubadilisha jina la jimbo au kugawa jimbo.

(3) Mapendekezo yaliyowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (2) yatazingatia utaratibu ufuatao:

(a) kuwasilishwa na kujadiliwa katika vikao vya halmashauri;
(b) kuwasilishwa na kujadiliwa katika kamati ya ushauri ya Wilaya;
(c) kuwasilishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa kwa ajili ya kujadiliwa katika Kamati ya Ushauri ya Mkoa; na
(d) kuwasilisha kwa Tume mapendekezo yaliyopitishwa na kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa pamoja na viambatisho vyote.

(4) Baada ya kupokea mapendekezo na viambatisho husika, Tume itafanya uchambuzi kujiridhisha endapo mapendekezo husika yamekidhi vigezo.

(5) Tume itatakiwa, kabla ya kugawa na kuanzisha jimbo jipya, kutembelea jimbo linalopendekezwa kugawanywa au kubadilishwa jina ili kujiridhisha endapo limekidhi vigezo.

(6) Tume, baada ya kujiridhisha kwamba jimbo linalopendekezwa kugawanywa au kubadilishwa jina limekidhi vigezo na masharti yaliyoainishwa chini ya Sehemu hii, itaomba kwa Rais kibali cha kugawanya jimbo au kubadilisha jina la jimbo.

(7) Tume baada ya kupata kibali cha Rais chini ya kanuni ndogo ya (6), itatangaza katika Gazeti la Serikali na vyombo vya habari orodha ya majimbo mapya.

## SEHEMU YA TISA
## MAADILI YA UTENDAJI YA TUME

Maadili ya utendaji kwa Wajumbe wa Tume

**18.-** (1) Kwa kuzingatia kifungu cha 11 cha Sheria na kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume, kila Mjumbe wa Tume atalazimika kuzingatia maadili ya utendaji wa Wajumbe wa Tume kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne.

Sura ya 398

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mjumbe wa Tume atalazimika kuzingatia Sheria ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma na sheria nyingine za nchi.

Maadili ya utendaji kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi
Sura ya 398

**19.-** (1) Kwa kuzingatia kifungu cha 18 cha Sheria na kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi atalazimika kuzingatia maadili ya utendaji kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi wa Uchaguzi atalazimika kuzingatia Sheria ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma na sheria nyingine za nchi.

## SEHEMU YA KUMI
## WATUMISHI NA WATENDAJI WA TUME

Watumishi wa Tume

**20.-**(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 20 cha Sheria, Tume, inaweza kuajiri, kuteua au kuazima kwa muda mtumishi kwa lengo la kutekeleza majukumu ya Tume.

(2) Mtumishi aliyeajiriwa, aliyeteuliwa au kuazimwa kwa muda atakuwa ni mtumishi halali wa Tume kwa kipindi chote atakachokuwa anatekeleza majukumu ya Tume.

(3) Watumishi wa Tume watalipwa posho na stahili nyingine kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu na miongozo itakayotolewa na mamlaka husika.

(4) Watumishi wa Tume watalipwa posho na stahili nyingine maalum kwa mujibu wa miongozo na nyaraka mbalimbali kama itakavyoamuliwa na Tume.

(5) Utaratibu wa kuazima mtumishi wa muda utafanyika kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Sura ya 298
Sura ya 2
Na. 1 ya 2024
Na. 2 ya 2024

(6) Mtumishi wa Tume katika kutekeleza majukumu yake atapaswa kuzingatia Katiba, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, sheria nyingine za nchi, miongozo, taratibu na maelekezo yatakayotolewa na Tume katika kipindi chote atakapokuwa anatekeleza majukumu ya Tume.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## WAJIBU WA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KWA WANANCHI

Elimu ya mpiga kura

**21.-(**1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria, Tume itakuwa na wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

(2) Tume inaweza, kabla na wakati wa mchakato wa uchaguzi au uandikishaji wa wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kualika taasisi na asasi za kiraia ili kushiriki katika kutoa elimu ya mpiga kura.

(3) Taasisi na asasi za kiraia zilizoalikwa chini ya kanuni ndogo ya (2) zitaomba

kibali kwa Tume kwa kufuata utaratibu ambao Tume itaelekeza.

(4) Baada ya kupokea maombi ya taasisi au asasi za kiraia, Tume inaweza kukubali au kukataa maombi hayo kwa kuzingatia vigezo vitakavyotolewa na Tume.

(5) Endapo Tume itakubali maombi, itatoa kitambulisho cha usajili kwa taasisi au asasi ya kiraia na barua ya utambulisho ambayo itapaswa kuwasilishwa kwa afisa mwandikishaji au msimamizi wa uchaguzi wa eneo analokwenda kutoa elimu.

(6) Kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya kanuni hii, Tume itaandaa mwongozo wa utoaji wa elimu ya mpiga kura utakaozingatiwa na taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura.

(7) Endapo Taasisi au asasi ya kiraia itakiuka masharti ya Sehemu hii, Tume inaweza kusitisha kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kilichotolewa kwa Taasisi au Asasi katika zoezi la uchaguzi au uboreshaji unaoendelea au kuizuia Taasisi au asasi husika kushiriki katika kutoa elimu ya mpiga kura katika mchakato wa uchaguzi au uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaofuata au vyote kwa pamoja.

Idhini ya maudhui yanayotumika kutoa Elimu ya mpiga kura

**22**.- (1) Taasisi au asasi ya kiraia inayokusudia kutumia zana au nyenzo kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura itatakiwa kuwasilisha Tume zana na nyenzo hizo ili kupata idhini ya Tume.

(2) Zana na nyenzo zitakazoandaliwa na taasisi au asasi ya kiraia zitapaswa kufuata Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura uliotolewa na Tume.

(3) Tume inaweza kukataa zana au nyenzo yoyote ambayo itakuwa kinyume na Sheria, kanuni, miongozo na maelekezo yaliyotolewa na Tume.

(4) Endapo Tume itaidhinisha au kutoidhinisha maudhui yanayotarajiwa kutumika katika kutoa elimu ya mpiga kura, itamtaarifu mwombaji kuhusu uamuzi huo.

(5) Tume itafanya ufuatiliaji wa tathmini kuhusu elimu ya mpiga kura inayotolewa na taasisi au asasi za kiraia wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## UHUSIANO KATI YA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI NA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Uhusiano wa Tume na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

**23**.- (1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 16 cha Sheria, katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(2) Ushirikiano kati ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar utajumuisha uendeshaji wa vikao vya pamoja.

(3) Bila ya kuathiri kanuni ndogo ya (2), Tume na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar zinaweza kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya uchaguzi kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## MASHARTI MENGINEYO

Masharti ya fedha

**24**. Kwa mujibu wa Kanuni hizi, gharama zitakazotumika katika Kamati ya Usaili na Kamati ya Uchunguzi zitalipwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

## MAJEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA

## NEMBO YA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 3)*

Ufafanuzi:

1. Alama katika Nembo:

(a) Ramani ya Tanzania inaashiria eneo la mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo uchaguzi hufanyika;

(b) Sanduku linaashiria jukumu linalotekelezwa na Tume la kusimamia na kuratibu zoezi la kupiga kura; na

(c) Mkono ukitumbukiza karatasi kwenye sanduku unaashiria haki ya kupiga kura.

(d) Sanduku la kupigia kura lenye rangi nyeupe, nyeusi au bluu zikiwakilisha masanduku ya kura za Diwani, Mbunge na Rais, mtawalia.

2. Rangi katika Nembo:

(a) Rangi ya pinki nzito inawakilisha rangi ya Tume ambayo haishabihiani na rangi za vyama.

(b) Nyeupe inaashiria uwazi wa Tume katika kutekeleza majukumu yake.

(c) Nyeusi inaashiria rangi ya mwafrika.

(d) Njano inaashiria rasilimali za nchi.

(e) Bluu inaashiria bahari na maziwa.

(f) Ua la ngano linawakilisha shughuli za kiuchumi hasa kilimo.

## JEDWALI LA PILI

UTARATIBU WA UTEUZI NA MAJUKUMU YA SEKRETARIETI YA KAMATI YA USAILI

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 9)*

1. Katibu wa Kamati atateua maafisa kutoka katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano wasiopungua watano kuwa wajumbe wa Sekretarieti, kupitia barua ya uteuzi kwenda kwenye mamlaka zao za ajira.
2. Sekretarieti itajumuisha wajumbe wafuatao:
   (i) mwanasheria na afisa mwingine mwenye uzoefu katika masuala ya uchaguzi;
   (ii) afisa tawala na afisa utumishi mwenye uzoefu katika kada husika; na
   (iii) maafisa kutoka kada nyingine kwa kadri Katibu atakavyoona inafaa.
3. Majukumu ya Sekretarieti yatakuwa kama ifuatavyo-
   (i) kuandaa matangazo ya nafasi wazi za Wajumbe au Mjumbe wa Tume;
   (ii) kupokea maombi ya waombaji kwa muda utakaoainishwa na Kamati ya Usaili;
   (iii) kufanya uchambuzi wa awali na kuwasilisha kwenye Kamati ya Usaili orodha ya waombaji waliokidhi vigezo pamoja na viambatisho husika;
   (iv) kufanya maandalizi ya usaili;
   (v) kuandaa taarifa ya matokeo ya usaili na kuiwasilisha kwa Kamati ya Usaili; na
   (vi) kutekeleza majukumu mengine kama itakavyoelekezwa na Katibu wa Kamati ya Usaili.

## JEDWALI LA TATU

### VIGEZO VYA UGAWAJI WA MAJIMBO

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 16)*

Kwa kuzingatia masharti ya Katiba na Sheria, katika kugawa mipaka ya majimbo ya uchaguzi, Tume itazingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye Katiba na vigezo vingine kama vilivyoainishwa katika Jedwali hili.

**A. VIGEZO VYA KIKATIBA**

(i) idadi ya watu;
(ii) upatikanaji wa njia za mawasiliano; na
(iii) hali ya kijiografia ya eneo husika.

**B. VIGEZO VINGINE VYA KUZINGATIA WAKATI WA UGAWAJI WA MAJIMBO**

(i) Wastani wa idadi ya watu
Wastani utapatikana kwa kuchukua jumla ya idadi ya watu nchini na kugawanya kwa jumla ya idadi ya majimbo ya wakati huo. Kigezo hiki kitazingatia tofauti ya idadi ya watu kati ya maeneo ya mjini na vijijini.

(ii) Hali ya Kiuchumi
Hali ya kiuchumi ya jimbo husika itazingatiwa kwa kuangalia idadi au asilimia ya watu wanaoishi chini ya asilimia ya mstari wa umaskini na mapato ya kodi ya jimbo husika.

(iii)Ukubwa wa eneo la jimbo husika
Jimbo ambalo lina eneo kubwa linaweza kugawanywa kwa kulinganisha na jimbo lenye eneo dogo.

(iv)Mipaka ya kiutawala
Katika kugawa jimbo, Tume itazingatia mipaka ya kiutawala iliyopo.

(v) Jimbo moja kutokuwa ndani ya wilaya au halmashauri mbili
Kigezo hiki kitazingatiwa ili kuzuia mbunge kuwakilisha wilaya au halmashauri mbili kwa wakati mmoja.

(vi)Mpangilio wa maeneo ya makazi ya watu yaliyopo
Kigezo hiki kitazingatia mpangilio wa makazi ya watu katika eneo husika.

(vii) Mazingira ya Muungano

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muunganiko wa nchi mbili ambazo ni Tanganyika na Zanzibar hivyo katika kugawa majimbo Tume itazingatia upekee wa mazingira ya muungano.

(viii) Uwezo wa Ukumbi wa Bunge
Kabla ya zoezi la kugawa majimbo halijaanza Tume itazingatia uwezo wa ukumbi wa jengo la Bunge.

(ix)Idadi ya Viti maalum vya wanawake
Katika kuamua kuongeza idadi ya majimbo, Tume itazingatia hesabu ya idadi ya viti maalum vya wanawake.

**C. FOMULA YA KUGAWA MAJIMBO**
Tume inaweza kutengeneza fomula ya vigezo vya ugawaji wa majimbo na kuviwekea uzito na kwa kuzingatia kipaumbele.

## JEDWALI LA NNE

## MAADILI YA UTENDAJI WA WAJUMBE WA TUME NA MKURUGENZI WA UCHAGUZI

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 18(1) na 19(1))*

**Utangulizi**

Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wanapaswa kufuata masharti yaliyoainishwa katika maadili haya, Katiba, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na Sheria ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma. Misingi ya Maadili kwa Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi inajumuisha yafuatayo:

1. **Uadilifu na uaminifu katika kutekeleza majukumu**

   Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wanapaswa kuwa wakweli na waaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuepuka mwenendo ambao unaweza kushusha hadhi ya Tume.

2. **Kutekeleza majukumu kwa weledi**

   Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa weledi ili kulinda hadhi ya Tume.

3. **Kufanya uamuzi kwa uhuru**

   Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wanapaswa kufanya uamuzi kwa uhuru bila kufuata maelekezo au amri kutoka taasisi yoyote ya Serikali, chama chochote cha siasa au mtu yeyote.

4. **Kuepuka mgongano wa maslahi**

   Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wanapaswa kuepuka mazingira yanayoweza kusababisha mgongano wa maslahi ya umma au binafsi katika kutekeleza majukumu ya Tume. Endapo kutatokea mgongano wa maslahi Mjumbe wa Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa kadri itakavyokuwa anatakiwa kuweka wazi mgongano huo na kujitoa kwenye mchakato wa uamuzi.

5. **Kuepuka vitendo vya rushwa**

   Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wanapaswa kuepuka vitendo vitakavyoashiria kupokea, kudai au kutoa rushwa wakati wa kutekeleza majukumu ya Tume.

6. **Kuepuka matumizi mabaya ya madaraka**

Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi hawapaswi kutumia madaraka yao vibaya wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

7. **Utunzaji wa siri**

Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi hawapaswi kutoa taarifa zozote za siri ambazo wamezifahamu kutokana na madaraka waliyonayo wakiwa kazini na baada ya ukomo wa majukumu yao.

8. **Kuepuka upendeleo**

Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi hawapaswi kufanya uamuzi kwa upendeleo kwa kuzingatia maslahi binafsi, kikundi cha watu, ndugu, kabila, dini, rangi, ukoo, utamaduni, jinsi, chama chochote cha siasa kinachoshiriki katika uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kufahamiana au vinginevyo wakati wa kutekeleza majukumu yao.

9. **Uwazi**

Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi wanapaswa kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu yao unafanyika kwa uwazi.

10. **Uwajibikaji**

Mjumbe wa Tume na Mkurugenzi wa Uchaguzi katika kutekeleza majukumu yao wanapaswa kuwajibika ipasavyo na kuzingatia Katiba, sheria na miongozo inayotolewa na Tume.

Dodoma,
……………., 2024

**JACOBS C. M. MWAMBEGELE**
*Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi*